AUSCO

Programu ya Maelekezo ya Kitamaduni nchini Australia

# Elimu ya Watu Wazima

Rahisi Kusoma

## Elimu kwa watu wazima nchini Australia



Katika Australia, watu huona kujifunza kama kitu ambacho wewe unaweza kufanya maishani yako yote.



Hata wakati wewe ni mtu mzima, wewe unaweza:

- kuendelea na mafunzo
- kujifunza
- kwenda shule kwa mara ya kwanza



Kujifunza kuzungumza, kusoma pamoja na kuandika katika lugha ya Kiingereza ni muhimu.



Hii itakusaidia wewe:

- kuhusika na maisha ya Australia



- kujihisi vizuri kuhusu maisha yako nchini Australia



- kutafuta kazi



- kukupa wewe fursa bora

## Kujifunza Kiingereza



Serikali hukusaidia wewe kujifunza Kiingereza kupitia kwa Programu ya Kujifunza Kiingereza kwa Watu Wazima Wahamiaji (Adult Migrant English Program - AMEP).



Hii haikugharamu pesa zozote.





Wewe unaweza kujifunza Kiingereza kwa hadi masaa 510.




Wewe unahitaji kujisajili kwa ajili ya AMEP ndani ya miezi 6 ya kwanza ambayo wewe upo nchini Australia.



Kuna huduma ya mtoto ya bure kwa watoto wadogo ambayo unaweza kutumia wakati unapoenda masomo.



Kuna njia tofauti za kushiriki katika AMEP kama wewe:

- ukihitaji kufanya kazi



- ukihitaji kutunza jamii yako



Wewe unaweza kuwa na uwezo wa:

- kusoma nyumbani



- kupata mwalimu atakayekutembelea nyumbani na kusaidia wewe



- kwenda kwenye masomo ya muda mfupi tu



- kwenda kwenye masomo baada ya masaa ya kazi ya kawaida




Wewe unaweza kupata maelezo zaidi kuhusu AMEP kwenye tovuti ya Idara ya Elimu na Mafunzo (Department of Education and Training).
[www.education.gov.au/amep](www.education.gov.au/amep)

# Masomo mengine



Watu wazima ambao wanataka kuendelea kusoma na kujifunza wana uchaguzi mwingi.

Watu ambao wanajifunza wanajulikana kama wanafunzi.




Unaweza kuwa na uwezo wa kupata msaada kutoka serikali ya kulipia gharama za kujifunza.

Hii itategemea:



- mapato yako – ni pesa kiasi gani unaweza kupata kutoka kazi




- mali – chochote unachokimiliki pamoja na pesa ulizonazo katika benki.



Wewe unaweza kupata habari zaidi kwenye tovuti ya Idara ya Huduma ya binadamu (Department of Human Services - DHS). [www.humanservices.gov.au](http://www.humanservices.gov.au)

## Kumaliza shule ya sekondari




Wewe bado unaweza kukamilisha masomo yako ya shule ya sekondari kama wewe upo zaidi ya umri wa miaka 18.





Shule ya sekondari mara nyingi inaitwa shule ya upili katika Australia.




Unaweza kusoma katika Chuo cha Ufundi na Elimu ya Juu (Technical and Further Education - TAFE).




Unaweza kufaulu na kupata Cheti cha IV.




Cheti IV ni sawa na kiwango cha elimu ya shule ya sekondari.

## Kujifunza ustadi au biashara



Kazi nyingine zinahitajika ujifunze ustadi fulani.

Hizi zinaitwa ufundi.



Ufundini pamoja na:

- useremala



- mabomba



- kurebesha nywele



- kuchunga mazingira ya bustani



- kufanya kazi katika biashara




- utalii



- mikahawa





Wewe unaweza kujifunza ustadi unayohitaji wewe kwa ajili ya biashara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (Vocational Education and Training - VET).




Wewe unaweza kufanya VET katika vyuo vya TAFE.




Wewe unahitaji cheti cha shule ya sekondari.



Wewe utahitajika kulipa ada kwa:

- kwenda masomo



- vitabu unavyohitaji

## Uanagenzi



Wewe unaweza kujifunza ufundi kupitia mafunzo ya uanagenzi.



Uanagenzi huwa ni pamoja na:

- kufanya kazi kazini
- kufanya mafunzo ya ujuzi wewe unayohitaji kufanya kazi hiyo



Wewe utaweza kufanya mafunzo kama unao ujuzi sahihi wa kuanza.



Baada yako kukamilisha masomo yako ya uanagenzi wewe utapata sifa ambazo zinatambulika kote nchini Australia.



Masomo ya uanagenzi hukuwezesha kupata fedha wakati wewe ni kujifunza.





Wewe unahitaji kulipa ada kwa masomo ambayo wewe huhudhuria kwa mafunzo. Ada hizi zitakuwa tofauti katika maeneo mbalimbali.




Wewe unaweza kupata maelezo zaidi kuhusu vyuo vya TAFE ambazo wewe unaweza kuhudhuria kutoka kwa mfanyikazi wa kesi yako au mpendekezaji wako.

## Kwenda chuo kikuu




Kuna aina tofauti ya vyuo vikuu vya Australia:

- umma
- binafsi



Wewe unaweza kuhudhuria chuo kikuu kama:


- mwanafunzi wa shahada
- mwanafunzi wa shahada ya juu

## Wanafunzi wa Shahada




Wanafunzi wa shahada ya kwanza ni wanafunzi ambao wanakwenda chuo kikuu kwa mara ya kwanza.

Vyuo vikuu vinazo:




- nafasi za kilipa sehemu – Serikali inasaidia kulipa ada





- nafasi za kulipia ada kamili – mwanafunzi hulipia gharama zote




Kutegemea kozi wanavyotoa, wanafunzi wapya wanaanza vyuo vikuu:

- Januari /Februari
- Julai/Agosti




Baadhi ya vyuo vikuu pia huwa na kozi wakati wa majira ya joto.



Ili kupata kujiunga na chuo kikuu huenda ukahitaji:

- kufanya mitihani




- kuonyesha Kiingereza chako ni kizuri



- kuthibitisha masomo gani umeshayafanya hapo awali




- kufanya kozi ya daraja ya elimu ya juu – masomo ya kukusaidia wewe kujitayarisha kwa masomo ya chuo kikuu




Ni gharama kubwa ya pesa ili kusoma katika chuo kikuu nchini Australia.




Programu ya Mkopo wa Elimu ya Chuo Kikuu (Higher Education Loan Program - HELP) inaweza kukusaidia wewe na gharama.



Ikiwa wewe hutumia HELP, unaweza kulipia masomo yako baada ya kumaliza – wakati wewe unapofanya kazi pamoja na wakati utakapopata pesa za kutosha.



Wewe unaweza kupata maelezo zaidi kuhusu HELP kwenye tovuti ya StudyAssist.
[www.studyassist.gov.au](http://www.studyassist.gov.au)

## Wanafunzi wa Shahada ya Juu



Wanafunzi wa shahada ya juu ni wanafunzi ambao hurudi chuo kikuu ili kufanya masomo ya ziada baada wamehitimu – kufaulu na kupata shahada ya kawaida.





Ikiwa wewe unaweza ulihitimu nje ya nchi, chuo kikuu kitaangalia sifa zako.

Idara ya Elimu na Mafunzo inaweza kukupa wewe maelezo kuhusu jinsi ya kupata shahada yako kutambuliwa nchini Australia.



Wewe unaweza kupata maelezo zaidi ikiwa wewe utatafuta 'Utambuzi wa sifa' (Qualifications recognition) kwenye tovuti ya Idara ya Elimu na Mafunzo.
www.internationaleducation.gov.au



Kunao uwezekano wewe kufanya kozi ya daraja ambayo itakusaidia wewe kupata sifa zako kufikia viwango vya Australia.

## Kwenda kwenye masomo na kozi za ziada



Wewe unaweza kupata kozi na masomo katika jamii yako kuhusu mambo unayotaka kujifunza.




Wewe unaweza kufanya hivyo katika:

- shule




- vyuo vya jamii




- TAFE




- vyuo vikuu



Hii inaweza kuwemo:


- upishi




- Kiingereza na lugha zingenezo



- kucheza densi



- upigaji picha



- ustadi wa kompyuta



- uwekaji wa hesabu – ili kusimamia pesa zako



- afya yako na ustawi wako



- ujuzi muhimu wa kikazi




Kozi hizi hazitoi sifa za rasmi.



Wewe unaweza kufanya aina hizi za kozi:

- baada ya masaa ya kawaida ya kazi




- wakati wa wikendi



Pia baadhi ya mashirika ya huduma za wahamiaji pamoja na ajenti za huduma huendesha kozi hizi.

## Elimu kwa jamii yote



Maktaba ya umma ya eneo lako ni sehemu nzuri kwa kupata taarifa.



Hii haikugharimu wewe chochote ili kujiunga na maktaba.

Wewe unaweza kukopesha:




- vitabu



- magazeti




- video na DVDs



- CDs




Maktaba nyingi huwa na:

- kompyuta ambazo wewe unaweza kutumia
- huduma ya bure ya mtandao



Wewe unaweza tu kuwa na uwezo wa kutumia kompyuta kwa muda mfupi.




Labda utahitaji kupanga muda wa kutumia kompyuta.




Ni muhimu kufuata kanuni za maktaba.




Wewe unahitaji kurejea vitu ulivyokopesha kwa wakati wake.

Ikiwa wewe hurudishi vitu kwa wakati unaofaa wewe unaweza kuulizwa kulipa faini ndogo.

# Utunzaji wa mtoto



Wewe unaweza kutumia huduma za utunzaji wa mtoto ikiwa unataka:

- kufanya kazi
- kusoma
- kwenda kujifunza kwa kikazi




Mfanyakazi wako au proposer anaweza kukusaidia kupata utunzaji wa mtoto unaofaa kwako.



Wewe unaweza kupata maelezo kuhusu huduma za utunzaji wa watoto na huduma za mafunzo ya mapema kwenye tovuti ya MyChild.
www.mychild.gov.au

Australian Government
Department of Social Services

Inaletwa kwako na Shirika la Uhamiaji la Kimataifa kwa niaba ya Idara ya Huduma za Jamii nchini Australia

IOM • OIM